# HALMASHAURI YA WILAYA YA IKUNGI

**SHULE YA SEKONDARI MUNKINYA**

**S.L.P 784**

**SINGIDA**

**MOB. 0756545455**

**TAREHE……………….**

**Kumb. Na. MSS/JI……………/20…………**

**Jina la Mwanafunzi**

**………………………………………………………**

**S.L.P………………………………**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUNKINYA WILAYA YA IKUNGI MKOA WA SINGIDA MWAKA 20…………**

## 1.0 UTANGULIZI

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Munkinya mwaka 20……….

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe ………………………….. unatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe ……………………… na mwisho wa kuripoti ni tarehe ………………………….

Mzazi ambaye atashindwa kumleta mtoto wake shuleni kwa tarehe tajwa hapo juu hatua kali zitachukuliwa dhidi yake ikiwa ni pamoja na kufikishwa mahakamani.

FMlelwa
…………………………………

**FARAJA G. MLELWA**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE
SHULE YA SEKONDARI MUNKINYA
S.L.P. 784 SINGIDA

## i) MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

Angalia jedwali na mchoro hapo chini. Aidha kitambaa cha sare kimeambatanishwa kikionyesha aina na rangi

| A. WAVULANA | B. WASICHANA |
|---|---|
| 1. Suruali 2 kijani mashono angalia mchoro chini<br> | 1. Sketi 2 kijani mashono angalia mchoro chini<br> |
| 2. Mashati 2 meupe mikono mifupi (tetroni) sweta la kijani<br>3. Viatu vyeusi vya ngozi (flat shoes)<br>4. Soksi nyeupe jozi 2 bila marembo<br>5. Michezo T-shirt njano bukta blue na raba nyeupe na soksi ndefu blue<br>NB: Sare ya Shule inavaliwa na tai ya kijani | 2. Mashati 2 meupe mikono mifupi (tetroni) sweta la kijani<br>3. Viatu vyeusi vya ngozi (flat shoes)<br>4. Soksi nyeupe jozi 2 bila marembo<br>5. Michezo T-shirt njano bukta blue na raba nyeupe na soksi ndefu blue<br>NB: Sare ya Shule inavaliwa na tai ya kijani |

## ii) VIFAA VYA DARASANI

a) Madaftari makubwa 10 (counter books) imependekezwa na madaftri madogo 9 kwa ajili ya mazoezi
b) Kibwete (mathematical set)
c) Faili moja kwa kumbukumbu za mwanafunzi
d) Kalamu, penseli, kifuto na rula
e) Uje na saa ya mkononi kwa ajili ya kutunza muda

Uje na begi la madaftari sio Rambo

## iii) KUCHANGIA CHAKULA CHA WANAFUNZI WA KUTWA.

Mzazi/Mlezi atalazimika kuchangia chakula cha mtoto wake kadri ya ya makubaliano ya vikao vya wazazi na shule kwa usimamizi wa Bodi ya shule na kamati ya wazazi iliyochaguliwa na wazazi wenyewe.

Vilevile mwanafunzi anatakiwa kuja na ufagio wa chelewa kwa ajili ya usafi

## iv) SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa na sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na Ofisi ya RAIS – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule lazima
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
d) Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nyingine utakazopewa
e) Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.

(f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira
(g) Kuvaa sare ya Shule wakati wote unapotakiwa
(h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na
(i) Kutunza mali za umma

3.1 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA MASOMO

a) Wizi
b) Uasherati na ushoga
c) Ubakaji
d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine,mirungi, kubeli na kadhalika.
e) Kupigana au kupiga
f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
g) Kudharau Bendera ya Taifa
h) Kuwa mjamzito/kupata mimba
i) Kuoa au kuolewa
j) Kutoa mimba
k) Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa Shule au watu
l) Kukataa adhabu kwa makusudi
m) Kuwa na simu ya mkononi

**3.2 MATIBABU**

Mwanafunzi ataripoti saa moja asubuhi kwa mwalimu wa zamu, ataandikwa kwenye daftari la wagonjwa na kwenda zahanati kutibiwa na kurudi shuleni. Iwapo hali yake haimruhusu kuendelea na masomo atapatiwa kibali na mganga na kuleta shuleni kwanza kisha ataruhusiwa kwenda kupumzika. Yule ambaye hali yake haimruhusu kufika shuleni Mzazi/Mlezi alete taarifa kwa Mkuu wa Shule na ataendelea kufanya hivyo mpaka mwanafunzi atakapopona na kumleta shuleni akiwa na vyeti vya matibabu.

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI**

a) Medical Examination Form ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali, fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakapo ripoti shuleni
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.

**Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu**

**KARIBU SANA MUNKINYA SEKONDARI**

Mlelwa

______________________

**FARAJA G. MLELWA**

**MKUU WA SHULE**

MKUU WA SHULE

**MAKUBALIANO KATI YA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI KWA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

1. Mimi Ndugu .......................................................Mzazi/mlezi wa ..................................... nimezisoma kwa makini sheria za shule hii. Nimezielewa na kuzikubali Naahidi kushirikiana na utawala wa shule kwa kuhakikisha kuwa mwanangu anazielewa, anazikubali na kuzifuata kwa dhati kwa muda wote atakapokuwa shuleni Nakubali kuwa mwanangu akishindwa au kukataa kufuata sheria hizo na asipojirudi baada ya kuonywa na walimu na walezi wake arudishwe nyumbani mara moja

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.......................................................................................

Tarehe ...................................................................................................................

2. Mimi ..................... nimekubaliana na mwongozo na sheria hizi na nitatekeleza maagizo yote wakati niwapo shuleni

Sahihi a mwanafunzi...................................................................................................

Tarehe ..................................................................................................................

Nakala ya kurudi shuleni

**MAKUBALIANO KATI YA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI KWA SHERIA NA TARATIBU ZA SHULE**

2. Mimi Ndugu .......................................................Mzazi/mlezi wa ..................................... nimezisoma kwa makini sheria za shule hii. Nimezielewa na kuzikubali Naahidi kushirikiana na utawala wa shule kwa kuhakikisha kuwa mwanangu anazielewa, anazikubali na kuzifuata kwa dhati kwa muda wote atakapokuwa shuleni Nakubali kuwa mwanangu akishindwa au kukataa kufuata sheria hizo na asipojirudi baada ya kuonywa na walimu na walezi wake arudishwe nyumbani mara moja

Sahihi ya Mzazi/Mlezi.......................................................................................

Tarehe ...................................................................................................................

Mimi ................................... nimekubaliana na mwongozo na sheria hizi na nitatekeleza maagizo yote wakati niwapo shuleni

Sahihi ya mwanafunzi...................................................................................................

Tarehe ..................................................................................................................

Nakala ya kurudi shuleni

MUKINYA SECONDARY SCHOOL BOX 784 SINGIDA

**TEL:** 0756 545455

MEDICAL EXAMINATION FORM

TO BE COMPLETED BY MEDICAL OFFICER

STUDENT'S FULL NAME ……………………………………………………………………………………………

DATE OF BIRTH ……………………………………………………………………………………………………

ADDRESS ………………………………………………………………………………………………………………

ESR ……………………………………………………………………………………………………………………

B/S……………………………………………………………………………………………………………………

T.B TEST…………………………………………………………………………………………………………

HB ……………………………………………………………………………………………………………………

VDRL…………………………………………………………………………………………………………………

STOOL EAMINATION ………………………………………………………………………………………

URINE ANALYSIS……………………………………………………………………………………………

EYE TEST…………………………………………………………………………………………………………

EARS…………………………………………………………………………………………………………………

CHEST………………………………………………………………………………………………………………

ASTHMA……………………………………………………………………………………………………………

ABDOMEN…………………………………………………………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION :PHYSICAL DEFFECTS, INFECTION, CHRONIC OR IMPAIRMENT

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………………

I CERTIFY THAT I HAVE EXAMINED THE ABOVE STUDENT AND RECOMMEND THAT /HE/SHE IS/ FIT/UNFIT TO PURSUE SECONDARY EDUCATION

| ………………………………… | ………………………… | ………………………… |
|---|---|---|
| DESIGNATION | SIGNATURE | DATE |

OFFICIAL STAMP